

**KANISA ANGLIKANA TANZANIA**

## **DAYOSISI YA SHINYANGA**



### **IBADA YA KUMWEKA WAKFU ASKOFU WA PILI WA DAYOSISI YA SHINYANGA**



**REV. CAN. CAPT. JOHNSON JAPHETH CHINYONG'OLE**

**KANISA KUU LA MTAKATIFU STEFANO, SHINYANGA**

***Wazo kuu: "Lisha Kondoo Zangu"***

**Jumapili ya 2 baada ya Ufunuo**

**14 Januari 2018**





**Askofu Charles Kijo Ngusa, askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Shinyanga**

## **DAYOSISI YA SHINYANGA**

Dayosisi ya Shinyanga ni sehemu ya Kanisa Anglikana Tanzania iliyokatwa toka Dayosisi ya Victoria Nyanza na kuzinduliwa Tarehe 20 Novemba, 2005. Askofu wa kwanza alikuwa Mhashamu Baba Askofu Charles Kija Ngusa aliyestaafu mwezi Novemba 2014.

Dayosisi ya Shinyanga iko Kaskazini Magharibi ya nchi ya Tanzania ikijumuisha Manispaa ya Shinyanga, Wilaya za Shinyanga vijijini, Kishapu, Maswa, Meatu, Itilima na Bariadi Mjini na Bariadi Vijijini katika Mkoa wa Simiyu zenye idadi ya watu wanazidi milioni Tatu na yenye wakristo Waanglikana Elfu sita.

## **MAONO**

Kanisa endelevu linalotumika pamoja kwa ufanisi wa ukuaji wa Ufalme wa Mungu kupitia maombi, ibada, kuhubiri na kufundisha.

## **UTUME**

Kutangaza Ufalme wa Mungu kwa ajili ya mabadiliko ya kiroho, kijamii na kiuchumi na uwezeshaji wa watu binafsi na jamii ili kupata uzoefu kamili wa maisha katika Mungu.

***Tumeitwa kutumika (Marko 16:15).***

Dayosisi ya Shinyanga inamiliki vituo na taasisi zifuatazo, Mwadui Anglican Primary School, Shule ya biblia Iselamagazi, Zahanati mbili za Solwana na Mwasingu ambazo kwa sasa zinaendeshwa na Halamashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Aidha Dayosisi ya Shinyanga ina vituo viwili vya huduma kwa watoto wanaotoka familia maskini navyo ni Anglican Shinyanga Student Center (TZ0336) Anglican Ndala Student Center (TZ0351).